
SautiElimu

hakielimu

Toleo la 3
2003

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org



Kutoka kwa mhariri

Na Rakesh Rajani

Toleo hili la SautiElimu linazungumzia usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za shule. Matumizi mazuri ya fedha za shule yanaleta ufanisi mkubwa; matumizi mabaya yanaathiri haki za watoto kupata elimu.

Katika hotuba yake ya tarehe 20 Septemba 2002, Rais Benjamin Mkapa alizungumzia jinsi Serikali ilivyoamua kubeba gharama za elimu ili kila mtoto hapa nchini aweze kupata elimu bure.

"…katika nchi yetu tunataka kila mtoto apate fursa sawa ya kujiendeleza hadi kikomo cha uwezo wake. Hatukubali umaskini uwe sababu ya mtoto kukosa fursa sawa. Ndiyo maana Serikali imeamua kubeba, kwa niaba ya wazazi, gharama za elimu ya msingi, ambayo itakuwa bora zaidi, kutoka katika bajeti yake."

Rais Mkapa aliendelea kueleza, "Ili kuzipa uwezo wa kifedha shule za msingi, iliamuliwa kwamba fedha zote za maendeleo, yaani za ujenzi wa majengo ya shule na za kufidia ada za shule, zitapelekwa moja kwa moja shuleni."

"Nimefahamishwa kuwa katika baadhi ya vijiji wananchi wamewawajibisha baadhi ya viongozi wa Kamati za Shule na walimu ambao walitaka kufanya matumizi mabaya ya fedha hizi. Huo ndio uwezeshaji halisi wa wananchi, ndio demokrasia ya kweli, na nawaomba wananchi wasisite kufanya maamuzi na kuwadhibiti watendaji wanaokiuka taratibu."

"Ilikuimarisha demokrasia, kila shule inawajibika kutoa taarifa ya mapato na matumizi kwa Serikali ya Kijiji au Mtaa kila baada ya miezi mitatu katika Mkutano wa Serikali ya Kijiji au Mtaa….Halmashauri na Shule wanawajibika kutoa matangazo kuhusu fedha zilizopokelewa, na matumizi yake, katika mbao za matangazo za Halmashauri, Shule na sehemu za mikusanyiko ya wananchi. Lazima sasa kila mwananchi ajue ni kiasi gani cha fedha kimepokelewa katika Halmashauri au shule yake, na jinsi zilivyotumika."

Je tunazingatia hayo?

Je unayafahamu haya?

Na Godfrey Telli

- Michango ya fedha yote ya lazima shuleni imefutwa lakini jamii inahamasishwa kushiriki kwa hiari na kujitolea nguvukazi.

- Taarifa za matumizi ya fedha zinatakiwa kuwa wazi kwa wanajamii wote wanaoizunguka shule pamoja na uongozi wa kijiji / mtaa.

- Fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) zinatoka Serikali Kuu (Hazina) kwenda kwa Serikali za Mitaa kabla ya kupelekwa moja kwa moja kwenye akaunti za kila shule.

- Kila shule ya msingi imefungua akaunti mbili katika benki ya NMB kwa ajili ya;

a) fedha zitolewazo kulingana na idadi ya wanafunzi walioandikishwa shule (capitation grant)

b) fedha kwa ajili ya maendeleo (development grant).

- Mwalimu mkuu anawajibika kuhakikisha mahesabu yote ya fedha yako sahihi na vitabu vya hesabu vinatunzwa vizuri.

- Katika awamu ya kwanza ya MMEM fedha zilizopatikana zilitumika zaidi kujengea miundombinu ya shule kama madarasa, nyumba za walimu na vyoo

- MMEM inajumuisha maeneo yafuatayo:
  - Uandikishaji wa wanafunzi darasa la kwanza
  - Ubora wa elimu
  - Utawala
  - Mafunzo kwa wadau ili kujenga uwezo.


- Kila shule ya msingi ina kamati ya shule yenye kuwajibika katika mapato na matumizi ya fedha shuleni.

- Kamati ya shule huchaguliwa kidemokrasia na kuundwa na wajumbe kutoka uongozi wa mtaa/kijiji, wanafunzi, wazazi, waalimu na wanajamii. Kamati ya shule inaratibu matumizi yote ya fedha za MMEM shuleni.



Michango shuleni itaendelea hadi lini?

Na Dotto Mfaume, Kivulini Mwanza



Serikali imefuta michango ya uandikishwaji wa watoto wa darasa la kwanza katika juhudi zake za kuboresha elimu ya msingi kwa kuhakikisha kila mtoto anakwenda shule na anapata elimu bora bila malipo.

Hatua ya serikali imekuja baada ya kuonekana kuwa kuna idadi kubwa ya watoto ambao hawapati elimu ya msingi kutokana na sababu mbalimbali lakini kubwa ni ukosefu wa ada miongoni mwa wazazi wasio na uwezo kifedha.

Cha kushangaza, pamoja na agizo hilo la serikali kuhusu kufuta michango bado inaendelea katika shule nyingi jijini Mwanza. Hali hiyo ni kikwazo kikubwa kwa watu wasio na uwezo na ambao walitegemea sasa wataweza kuwapeleka watoto wao shuleni kwa matumaini ya kupata elimu hiyo bure.

Baadhi ya wazazi walilazimika kurudi na watoto wao nyumbani baada ya kushindwa kulipia michango ya shule kabla ya kuwaandikisha. Fedha zilizotozwa ni kati ya shilingi 2,000/= hadi 3,000/=.

Kwa hali hiyo, ni vema hatua muhimu zikachukuliwa kwani athari zake ni kubwa kwa jamii na taifa. Je ni hatua zipi zifuatwe ikiwa mzazi anaombwa michango kwanza ili mtoto wake aandikishwe? Kuwaona viongozi peke yake haisaidii kwani baadhi yao wanakubaliana na hivyo vikwazo! Kwanini tuwaache watoto wetu wakose elimu kutokana na ufahamu mdogo au uzembe unaofanywa na watu wachache?

Ikiwa suala hili halitapatiwa ufumbuzi wa haraka hakutakuwa na haki sawa katika kupata elimu. Waathirika wengi wataendelea kuwa watoto wa kike ambao bado jamii haiamini kuwa wana uwezo sawa na watoto wa kiume kielimu. Baadhi ya wazazi huweza kutumia vigezo vya ukosefu wa ada kuwaacha watoto wa kike majumbani au kuwaoza wakiwa na umri mdogo!

Sera ya elimu haifahamiki kwa walengwa!

Na Marjorie Mbilinyi

Imeelezwa kuwa sera mpya ya elimu haifahamiki kwa wananchi wengi, wakiwemo walimu na baadhi ya watendaji. Hayo yalielezwa na washiriki katika moja ya Midahalo ya saa 1:30 asubuhi iliyoanzishwa ili kuwapa nafasi watu kutoka kada mbali mbali kujadiliana kuhusu masuala ya sera.

Walisema kutokuwa na mikakati shirikishi ya usambazaji wa habari, kukosa utawala bora wenye sifa za uwazi na uwajibikaji ni baadhi ya mambo yanayosababisha sera zinazoundwa kutowafikia walengwa hasa wananchi waliopo vijijini.

Wakichangia mjadala, washiriki waliichambua Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Ilielezwa kwamba kila shule ya msingi ilipewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na madawati. Fedha zingine zilitolewa kwa ajili ya kuboresha mafunzo ya walimu, ununuzi wa vitabu, n.k.

Kwa mujibu wa washiriki hao, matatizo na migongano ya maamuzi yamejitokeza katika ujenzi wa madarasa, motisha na maslahi ya walimu na mfumo wa serikali za mitaa kutokana na wananchi kutoelewa sera mbalimbali.

Ilipendekezwa kwamba kuwe na taratibu za kuhakikisha kuna mfumo wa usambazaji habari kutoka chini kwa wananchi hadi juu, na juu hadi chini. Washiriki walihimiza uwajibikaji wa viongozi na watekelezaji katika ngazi zote.

Midahalo hiyo ya saa 1.30 ilianzishwa na Business Times na NGO Policy Forum na inaendeshwa na HakiElimu. Midahalo hufanyika kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi. Washiriki ni waunda sera kutoka serikali, taasisi za maendeleo za ndani na nje ya nchi, asasi zisizo za serikali, vyombo vya habari na watu binafsi.

Mada katika mdahalo wa kwanza ilikuwa 'Tunafahamu nini kuhusu fedha katika ngazi ya shule?' Watoa mada walikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bw. Lyimo na Mratibu wa MMEM -TAMISEMI, Bw. Mtui.



SautiElimu

hakielimu

Toleo la 3
2003

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Ujumbe wa elimu kupitia kwenye vituo vya mabasi

Na Lilian R. Kallaghe



Mwalimu Nyerere alitoa mchango mkubwa katika sekta ya elimu nchini. Katika moja ya hotuba zake Mwalimu alieleza kuwa elimu inayotolewa inatakiwa kuwaandaa vijana kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa…

Ili kuenzi ushauri wake, HakiElimu imetengeneza vituo vya mabasi vyenye ujumbe mbalimbali uliotolewa na Mwalimu siku za uhai wake. Vituo hivyo vimewekwa sehemu mbalimbali nchini.

Kama umeviona vituo hivyo vya mabasi, tuandikie; Umeona lini? Wapi? Ni ujumbe gani ulioko katika kituo ulichoona? Tupe maoni yako!

Zawadi ya fulana za HakiElimu itatolewa kwa washiriki 50 watakaochaguliwa kwa njia ya bahati nasibu. Tuandikie kabla ya Septemba, 2003.



Harakati za Marafiki kuboresha elimu

Na Mary Nsemwa

Harakati za Marafiki wa Elimu ni mbinu nzuri ya kushirikisha jamii kuchangia maoni na kubadilishana uzoefu.

Hayo yalisemwa na mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Ilala, Joyce Chingalame, wakati wa uzinduzi wa Harakati za Marafiki wa Elimu, uliofanyika Machi 25 2003, katika Shule ya Msingi ya Buyuni iliyoko Kata ya Chanika, Ilala jijini Dar es Salaam. Harakati hizo zinalenga kuwaunganisha wananchi katika kuchangia maoni, kufuatilia na hatimaye kuboresha elimu nchini.

Bibi Chingalame aliendelea kusema ushiriki wa wananchi katika mambo yanayowahusu ni moja ya vipengele muhimu vya utawala bora. Ili kufanikisha Harakati hizo alihimiza umuhimu wa kila mdau kutimiza majukumu yake katika kuboresha elimu.

Akizungumzia Harakati hizo, mwakilishi wa ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo inaratibu shughuli za elimu nchini, Yokobety Malisa alisisitiza umuhimu wa ushiriki wa walengwa katika kuibua masuala muhimu yanayohusu uboreshaji elimu hapa nchini.


Naye mwakilishi wa Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Ezekiah Oluoch alisema kutowapa motisha walimu kumesababisha elimu bora inayohitajika sana kwa wanafunzi nchini kugeuka kuwa bora elimu.

Aliendelea kusema kwamba kuwa na majengo mazuri ya shule pekee bila kuzingatia ufundishaji bora kutaathiri mpango mzuri uliowekwa na serikali wa kuboresha elimu. Ili kupata elimu bora, Bw. Oluoch alisisitizia suala la motisha kwa walimu hapa nchini lipewe kipaumbele hasa katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM).

Serikali imezindua MMEM katika juhudi zake za kuhimiza ushiriki zaidi wa umma katika utawala wa shule. Kwa kuzingatia MMEM, Harakati za Marafiki wa Elimu zitatoa fursa kwa ajili ya upashanaji habari, kujifunza, uwajibikaji na uwazi katika ngazi zote za mfumo wa elimu. Hata katika hotuba zake, Rais Mkapa amekuwa akisisitiza uwazi na uwajibikaji, umuhimu wa wananchi kupata habari na kutoa maoni juu ya maendeleo yao.

HakiElimu ni mraghabishi wa Harakati za Marafiki wa Elimu. Mtu yeyote anaweza kuwa Rafiki wa Elimu! Hakuna masharti yoyote na uanachama ni bure. Marafiki wakijiunga watapokea kifungashi cha habari na muda wote wa uanachama wao watatumiwa habari zingine mara kwa mara pia watahimizwa kuwapasha habari hizo watu wengine katika jamii zao.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na HakiElimu kwa SLP 79401, DSM, barua pepe: rafiki@hakielimu.org au tovuti www.hakielimu.org



HakiElimu ni Shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika elimu kwa kuwezesha jamii kubadili shule na mfumo wa uundaji sera za elimu, kuimarisha ubunifu wa uendeshaji wa mijadala na midahalo ya umma, kufanya utafiti yakinifu, wenye kuhoji, kuchambua, kutetea na kushirikisha wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Shukurani kwa Shirika la kimataifa la kuhudumia watoto UNICEF, Alliance Media na Mwalimu Nyerere Foundation kwa msaada wa picha.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yeyote ya kijitabu hiki kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala kwa HakiElimu.

ISSN 08568588

© HakiElimu, 2003

Mhariri: Rakesh Rajani

Timu ya SautiElimu: Mary Nsemwa, Lilian R. Kallaghe, na Godfrey Telli.
Mchoraji: Marco Tibasima

Tuandikie!

HakiElimu, SautiElimu
SLP 79401
Dar es Salaam
Simu: 022 2151852 / 3
Faksi: 022 2152449
Baruapepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org



Ukurasa wa 2

Barua kwa SautiElimu

Mhariri SautiElimu, Napenda kutoa maoni yangu kuhusu mambo yanayochangia kuwepo kwa matokeo mabaya katika shule zetu.



Baadhi ya mambo yanayochangia kudumaza elimu ni idadi ya shule kuwa chache na mbali kutoka maeneo wanayoishi watu. Hali hiyo husababisha watoto kutembea umbali mrefu kufuata shule. Matatizo mengine ni pamoja na uhaba wa vifaa vya kujifunzia pamoja na madawati.

Napendekeza wazazi washiriki kwa karibu zaidi katika ujenzi wa madarasa, kuchangia ununuzi wa madawati na vifaa vya kufundishia. Vilevile walimu zaidi waajiriwe na kulipwa mishahara inayolingana na ugumu wa kazi yao.

Nashauri pia wazazi, wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla kujitolea zaidi katika masuala yanayohusu elimu.

Cassian P. Mangi
c/o SAUT
Box 307
Mwanza

•••

Mhariri SautiElimu, Utawala bora unaofaa katika elimu ni ule ambao ni shirikishi. Kwa maoni yangu, ili kuboresha elimu nashauri wazazi wahusishwe katika kutoa mawazo yao jinsi gani shule iendeshwe.
Wazazi na wananchi katika jumuiya inayozunguka shule wawe na tabia ya kuhoji juu ya mapato na matumizi ya fedha na mali zote za shule.
Pamoja na hayo, uongozi wa shule usitumie mabavu katika kudai fedha za michango na makusanyo kutoka kwa wazazi. Iwapo wazazi wataamua kuchangia kwa hiari yao, takwimu za matumizi ziandikwe kwa usahihi na uwazi.

Twilumba Mgohamwende
Sekondari ya Central
Dodoma

•••

Mhariri SautiElimu Mpango wa Elimu kwa walioikosa (MEMKWA) bado una utata mkubwa miongoni mwa jamii. Kwa maoni yangu, mpango huo unawabagua na kuwaadhibu watoto ambao walishindwa kuandikishwa shule kutokana na uwezo mdogo wa wazazi wao.

Suala la kuwabagua watoto hao na kuwapangia madarasa tofauti na wenzao lingefaa kuepukwa. Kwa mfano, mtoto mwenye umri wa miaka 13, kama ataendelea na masomo yake moja kwa moja hadi kupata shahada ya chuo kikuu atamaliza akiwa na miaka 30 tu!
Sasa umri huo umepindukia wapi kiasi cha kijana kushindwa kulitumikia taifa lake? Natoa mwito kwa Wizara ya Elimu kuwaandikisha watoto wote sawa, katika madarasa ya kawaida, bila kujali umri, hali ambayo inawabagua bila makosa. Bora kukawia lakini wafike.

Juma W. Kalwani
c/o Dr. Renatus Masangi
SLP 451
Bunda
Mara

•••

Mhariri SautiElimu, Mimi ni mzazi wa mtoto anayesoma katika shule moja ya msingi manispaa ya Dodoma. Kinachonitatiza ni kwamba kila mara kabla ya kufanya mitihani walimu wa shule hiyo wamekuwa wakidai sh. 100 kwa kila somo kutoka kwa wazazi wa wanafunzi. Fedha hizo zinaelezwa kuwa ni gharama ya kutoa nakala za maswali ya mitihani. Ninavyofahamu ni kwamba serikali imefuta michango ya lazima labda iwe midogo midogo tena ya kujitolea.
Sipingi kuchangia fedha hizo ila nahoji kwanini tuchangie kiwango hicho kikubwa cha sh. 100 kwa kila mwanafunzi wakati gharama halisi ya kutoa nakala moja ni sh. 30? Je fedha zinazosalia zinakwenda wapi ukizingatia shule ina wanafunzi 1,500?

Mzazi
Manispaa ya Dodoma

•••

Mhariri SautiElimu, Napenda kutoa pongezi kwa matangazo yenu yanayorushwa kwa njia ya televisheni. Matangazo hayo yamegusa mambo muhimu sana na maisha ya mtoto kielimu hapa Tanzania ambayo kwa kweli ni magumu.
Ombi langu ni kwamba ongezeni matangazo yanayogusa adhabu zisizo na msingi kwa wanafunzi kama vile viboko na kusitishwa masomo kwa muda (suspension) nk.

Luteni Solo
Email: solo45@darhotwire.com

Wiki ya Elimu Duniani 2003 (6-13 Aprili 2003)

Na Lilian R. Kallaghe



Kila mwaka dunia inaadhimisha Wiki ya Elimu. Mashirika mengi na watu binafsi kote duniani wanashiriki na kutumia wiki hii kama fursa ya kuhamasisha kuhusu masuala mbambali ya elimu.

Mwaka huu maadhimisho ya wiki hiyo yalilenga umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike. Msingi wa lengo hilo ulitokana na maazimio ya kamati iliyopitishwa na Mkutano wa Elimu wa Dunia (World Education Forum) kukuza Elimu kwa Wote (EFA).

Kamati hizi ziliazimia kwamba hadi kufikia mwaka 2005 wasichana wote wataweza kupata elimu bora ya msingi na kwamba ubaguzi wa kijinsia utakomeshwa katika elimu.

Wiki ya Elimu Duniani ni moja kati ya matukio yanayoandaliwa katika kampeni ya kimataifa kwa ajili ya elimu. Lengo kuu ni kuhamasisha jamii kutoa maoni na kushinikiza serikali zao na taasisi husika kutoa elimu bora na bure kwa wote.

Ulizia mashirika au vikundi mbalimbali katika jamii yako yalifanya nini katika kuadhimisha wiki hii!

Kama mwanajamii unaweza…

- Kuandaa midahalo katika jamii yako kuhusu changamoto zinazowakabili wasichana katika mfumo wa elimu nchini
- Kuuliza wanafunzi wa kike; Hali ikoje katika shule zao?
- Kuuliza Mwalimu Mkuu, Kamati ya shule au wawakilishi wa serikali za Mtaa/Kijiji; wanafanya nini kuongeza ushiriki wa wanafunzi wa kike katika shule?
- Kuchangia mawazo yako na wengine kwa kuandika barua kwenye vyombo vya habari
- Kuandika kwa SautiElimu



Tunapokea maoni kuhusu kuboresha jarida letu. Tutumie maoni yako! Ikiwa tutayatumia maoni hayo katika machapisho yetu tutakuzawadia fulana ya HakiElimu.